



CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY

# Ijue Mifuko ya Uwekezaji ya Pamoja (Collective Investment Schemes)



CMSA

1/5/2020

## YALIYOMO

1.0.	SOKO LA MTAJI NI NINI? .....	1
2.0.	MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA NI NINI?.....	1
3.0.	NAMNA MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA UNAVYOFANYA KAZI.....	2
3.1.	Lengo.....	2
3.2.	Meneja wa Mfuko .....	2
3.3.	Mwangelizi au Mdhamini wa Mfuko (Trustee/Custodian) .....	2
3.4.	Thamani ya Vipande.....	3
4.0.	FAIDA ZA MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA .....	4
5.0.	UWEKEZAJI WA PAMOJA UNAVYONUFAISHA WANANCHI KIUCHUMI .....	6
6.0.	USHAURI KWA UWEKEZAJI WA PAMOJA.....	7

## 1.0. SOKO LA MTAJI NI NINI?

Masoko ya Mitaji ni sehemu ya mfumo wa sekta ya fedha unaoweza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo ya muda mrefu yaani zaidi ya mwaka mmoja.

Fedha za maendeleo za muda mrefu huweza kupatikana kwa kuuza hisa za kampuni (shares), hatifungani za kampuni (corporate bonds), hatifungani za serikali (Government Bonds), hatifungani za serikali za mitaa (Municipal Bonds), na vipande katika uwekezaji wa pamoja (collective investment schemes).

Jukumu kuu la masoko ya mitaji ni kuwezesha upatikanaji wa fedha kutoka kwa wawekezaji na kuzipeleka kwenye uzalishaji na hivyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Washiriki wa masoko ya mitaji wako katika pande mbili – upande wa watoa dhamana yaani 'issuers' na upande wa wawekezaji yaani 'investors'.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ina jukumu la kuendeleza na kusimamia masoko ya mitaji na dhamana hapa nchini.

## 2.0. MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA NI NINI?



Mfuko wa uwekezaji wa pamoja ni mipango ya uwekezaji wa pamoja inayojumuisha ukusanyaji au uwekaji wa rasilimali pamoja kutoka katika wawekezaji mbali mbali na kuziwekeza rasilimali hizo kwenye amana mbali mbali.



Hapa Tanzania mifuko ya uwekezaji wa pamoja huanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Soko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79.

### **3.0. NAMNA MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA UNAVYOFANYA KAZI**

#### **3.1. Lengo**

Lengo la uwekezaji kwenye mfuko wa uwekezaji wa pamoja ni maalumu ambalo ni kuwekeza katika amana zinazouzika.

Lengo hili huwapa wawekezaji faida ya ukwasi ambayo ni muhimu. Kwa hiyo katika Mfuko wa namna hii, mwekezaji anaweza kununua na kuuza vipande (units) kwa Meneja wa Mfuko muda wowote anaotaka.

Mauzo na manunuzi yanaendelea kwenye muda wa biashara wakati wowote.

#### **3.2. Meneja wa Mfuko**

Jukumu la Meneja wa Mfuko wa Uwekezaji wa pamoja ni kuendesha mpango wa uwekezaji kwa mujibu wa wa Waraka wa Uundwaji wa Mfuko (Trust Deed) na kwa maslahi ya wawekezaji;

Ataandaa mahesabu ya fedha ya mfuko wa uwekezaji wa pamoja kwa mujibu wa sheria.

Atahakikisha kuwa nyaraka muhimu zinawekwa wazi kwa ajili ya kuangaliwa na wawekezaji na umma kwa ujumla.

Meneja huyu huingia mkataba maalum (nyaraka za udhamini) na mtunzaji maalum wa Mfuko (kwa lugha ya kigeni akiitwa "Custodian").

Meneja wa Mfuko ni msimamizi wa uwekezaji wa mali za mfuko na siyo mwana kikundi au mbia.

Hufanya shughuli zake kitaaluma kulingana na sheria.

#### **3.3. Mwangalizi au Mdhamini wa Mfuko (Trustee/Custodian)**

Ni msimamizi mkuu wa mfuko wa uwekezaji wa pamoja. Kazi zake ni pamoja na hizi zifuatazo:




- a. Kutunza, kuendesha au kufanya mipango ya uwekezaji kwa njia ile itakayoongeza thamani, faida au mapato yake.
- b. Kuwekeza, kupata, kutunza na kutoa amana na kutumia uwezo na haki zinazotokana na amana hizo.
- c. Kutoa mikopo yenye rehani ya mali yoyote isiyohamishika na inayohamishika.
- d. Kununua kuuza au kutoa hati za ushiriki kuhusiana na mkopo wowote, au fedha zilizotolewa na taasisi ya fedha au benki au taasisi nyingine ya namna hiyo.
- e. Kuwekeza katika hati yeyote maalum au amana iliyotolewa na Serikali, Benki Kuu au Serikali za mitaa.
- f. Kubuni kuhusiana na Mfuko wowote wa uwekezaji wa pamoja;
- g. Uwekaji wa akiba na mipango ya bima au mipango ambapo mtu anaweza kupata riba katika kushirikiana na kampuni ya bima lakini isiyojumuisha biashara ya bima.
- h. Mfuko mwingine wowote au mipango itakayomwezesha mtu kupata riba katika units.
- i. Kufanya aina yoyote au biashara inayohusu ukusanyaji wa akiba au uwekezaji ambao mwekaji wa mali katika dhamana anaweza kuruhusu;
- j. Kufanya kwa ujumla matendo yote na vitu vitakavyojitokeza au kutokana na utendaji wa kazi zake chini ya amana.

#### **3.4. Thamani ya Vipande**

Ni rahisi kupata thamani ya uwekezani wakati wowote maana tathmini hufuata thamani halisi ya rasilimali zilizopo.

Kwa kawaida uthamini huu hufanywa kila siku ya biashara.





#### 4.0. FAIDA ZA MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA



Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja inatoa faida zifuatazo:

- a. Kuwezesha upatikanaji wa mitaji mikubwa kwa njia ya kukusanya akiba ndogo ndogo kwenye mfuko mmoja (pooling resources into a fund):





- i. Badala ya kila mtu kuweka nyumbani TZS. 50,000/= kwa sababau ni kidogo sana kuwekezwa, watu 5,000 wangewekeza kiasi hicho na kujenga mfuko mkubwa wa kiasi cha TZS. 250,000,000/=
    - ii. Fedha zilizopo kwenye mfuko huu huwekezwa na faida inayopatikana kugawanywa kwa wale wawekezaji wadogo wadogo kulingana na kiasi walichowekeza.
  - b. Kupata faida zitokanazo na matumizi ya utaalamu wa usimamizi wa fedha kutoka kwa Meneja wa Mfuko:
    - i. Kuwekeza kwenye mfuko unaoendeshwa kitaaluma huhakikisha kwamba fedha zinawekezwa ipasavyo kwa faida ya waekezaji.
    - ii. Meneja mwenye taaluma huweza kutengeneza mchanganuo wa uwekezaji ambao unapunguza wasiwasi wa hasara (risk).
  - c. Kupata anuwai ambayo inaondoa na kupunguza vihatarishi (risks) vya kuwezekeza rasilimali zote kwenye aina moja ya biashara kwa kuwekeza fedha zilizokusanywa kwenye miradi ya aina mbalimbali:
    - i. Dhana ya Mifuko ya uwekezaji ni “usiweke mayai yote kwenye kapu moja”.
    - ii. Kama mwekezaji akiwekeza kwenye dhamana moja tu, ikipata hasara basi ni hasara ya moja kwa moja. Lakini akiwekeza kwenye dhamana mbali mbali basi hasara katika moja inaweza kufutwa na faida kutoka kwa nyingine.
  - d. Kupunguza gharama za uwekezaji (lower transaction costs) kwani wawekezaji wengi hutumia utaalamu wa meneja mmoja na hivyo kuongeza faida;
    - i. Mwekezaji binafsi mwenye fedha chache hulipa gharama kubwa zaidi za uwekezaji kuliko Meneja mwenye mfuko mkubwa na taaluma ya uwekezaji. Meneja huyu huweza kulipa kamisheni ndogo na vile vile huweza kupata riba kubwa zaidi kutoka kwenye taasisi za fedha.



- e. Huleta uwezo wa kufikia uwekezaji wa viwango vya juu (access to investment in higher thresholds):
- ii. Mwekezaji mwenye TZS. 50,000/= hawezi kuwekeza kwenye uwekezaji unaohitaji kwa uchache TZS. 1,000,000/=. Meneja aliyekusanya fedha kutoka kwa wawekezaji wengi na aliye na mfuko mkubwa huweza kufanya hivyo.
  - iii. Uwekezaji wa pamoja unaweza kufanikisha kuundwa kwa chombo maalum cha kukopesha fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa nyumba. Hii itasaidia wananchi wanaoshindwa kukopa kwa sababu ya kukosa mtaji wa mwanzo wa kuanzisha mradi.

## **5.0. UWEKEZAJI WA PAMOJA UNAVYONUFAISHA WANANCHI KIUCHUMI**

Mipango ya uwekezaji wa pamoja huenda sambamba na sera ya Serikali ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Uwezeshaji huu unahusiana na ushiriki wa makundi ya jamii katika uchumi wao na maendeleo endelevu yanayotokana na upatikanaji wa faida kutoka kwenye shughuli za kiuchumi kwenye jamii husika. Namna mahsusi ambazo uwekezaji wa pamoja unawawezesha wananchi kiuchumi ni kama ifuatavyo:

- a. Inawawezesha watu wa kipato cha chini kuwekeza rasilimali ndogo ndogo walizonazo. Kipengele hiki siyo tu kinatoa matumaini mahali pa kukata tamaa kwa wawekezaji wadogo, bali pia kinatoa nafasi ya kupatikana faida za kiuchumi baada ya muda. Faida kutoka katika mipango hii ya uwekezaji, inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha uwekezaji akiba kwa wale wenye vipato vidogo.
- b. Inaleta ushindani sawa katika mikakati ya kiuchumi kati ya wawekezaji wote wakubwa pamoja na wadogo kwa kuwafanya wawekezaji wadogo kuwekeza kwa viwango vya juu ambavyo vinatumia na wawekezaji wa kipato cha juu. Kwa hali hiyo faida





inayotolewa kwa wawekezaji wa kipato cha chini na Mfuko wa uwekezaji wa pamoja ni kubwa.

- c. Mipango ya uwekezaji wa pamoja inatoa fursa kwa mwekezaji kuwekeza kutegemea na vivutio vilivyopo na kupata faida. Faida inaweza kuwa katika mgawanyo wa kipato (income distribution) au inaweza kuchukua mfumo wa uongezaji thamani ya mtaji (capital appreciation). Katika Mpango wa mgawanyo wa kipato wawekezaji wanapata fursa ya kuwekeza tena kiasi walichopata katika mfuko huo au katika miradi mingine watakayoona inafaa na hata kutumia kwa matumizi mengine. Katika mpango wa uongezaji thamani ya mtaji, wawekezaji ambao wana malengo ya kuwekeza kwa muda mrefu, hupata faida ya kuongezeka kwa uwekezaji wao.
- d. Mwekezaji katika Mfuko wa uwekezaji wa pamoja anastahili kupata amana zinazoitwa vipande (units). Vipande hivi vya uwekezaji vinaweza kuhamishika na vinaweza kutumika kama rehani (collateral) ili kumwezesha mwekezaji kupata mkopo. Hili ni muhimu hususan pale washiriki mmoja mmoja wa makundi ya jamii wenye vipande wanapotaka kuendesha miradi katika maeneo yao. Inawezekana vipande vyao vya uwekezaji vikakusanywa ili kufikia thamani ya kudhamini miradi mikubwa.

## **6.0. USHAURI KWA UWEKEZAJI WA PAMOJA**

Kama ilivyoainishwa hapo juu, mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaweza kuleta faida kwa washiriki na kuwawezesha kiuchumi. Katika kufikia azma hiyo, ni muhimu kuzingatia ushauri wa wataalamu.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kama msimamizi wa masoko ya mitaji nchini ikiwa ni pamoja na mipango ya uwekezaji wa pamoja, inapenda kushauri wananchi na wawekezaji walio na azma ya kuanzisha mfuko wa uwekezaji wa pamoja kama ifuatavyo:



- a. Kuwa na waraka wa kisheria wa kuundwa kikundi cha uwekezaji kama vile Katiba ya Umoja au Memorandum and Articles of Association ikiwa mtaamua kuunda kampuni;
- b. Kuwa na Mpango Kazi wa Muda wa Kati wa kikundi (Medium Term Work Plan);
- c. Ikiwezekana, kupata usajili kama kampuni ya uwekezaji;
- d. Kufungua akaunti benki kwa ajili ya kikundi;
- e. Kukusanya mtaji kutoka kwa wanahisa / wanakikundi kwa kiwango cha uchangiaji na muda mtakaokubaliana na kadiri ya uwezo wa wanakikundi.
- f. Kampuni hiyo ya uwekezaji itatengeneza sera ya uwekezaji itakayojikita kwenye uwekezaji kwenye masoko ya mitaji kama vile mfuko wa uwekezaji wa pamoja. Jambo hili linaweza kufanywa hata kabla ya kuunda kampuni.
- g. Kuwasiliana na CMSA ambapo CMSA itawaunganisha na mmoja wa meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja kama vile UTT AMIS PLC ambaye amepewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kusimamia mifuko ya uwekezaji wa pamoja.
- h. Wapo mameneja wengine waliopewa leseni na Mamlaka lakini UTT AMIS wana uzoefu wa kutosha katika kusimamia mifuko ya uwekezaji wa pamoja na tayari wana mifuko 6 ambayo inafanya vizuri. Mifuko iliyo chini ya UTT ni Watoto Fund, Wekeza Maisha, Ukwasi, Jikimu, Umoja Fund na Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund).
- i. Kwa kushirikiana na Meneja wa Mteule wa Mfuko, kikundi kitaweza kufanya yafuatayo:
  - i. Kuanzisha mfuko ya uwekezaji wa pamoja;
  - ii. Kujenga uwezo wa wanahisa kwa njia ya elimu na mafunzo;
  - iii. Kufanya maendeleo ya miundombinu;
  - iv. Kutoa elimu kwa umma;
  - v. Kuweka muundo ambao ni wa wazi kuhusiana na uwajibikaji kwa shughuli za Mfuko.



- vi. Kujenga uwezo wa kujiendesha. Hii ina maana kwamba Wanakikundi watakuwa na uwezo wa kujiendesha kama asasi za kibiashara baada ya muda fulani.
- vii. Kampuni hii ikishafikia uwezo mkubwa itaweza kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.



**UWEKEZAJI WA PAMOJA UNAWEZESHA  
UTEKELEZAJI WA UCHUMI WA  
VIWANDA!**





**CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY**

**CHIEF EXECUTIVE OFFICER**

**Capital Markets and Securities Authority**

**6<sup>th</sup> Floor, PSSF Tower, Ohio and Garden Avenue,**

**P.O.Box 75713 Dar es Salaam,**

**Tel: +255 22 2114959 / 61**

**Fax: +255 22 2113846**

**Email: [info@cmsa.go.tz](mailto:info@cmsa.go.tz)**

**Website: [www.cmsa.go.tz](http://www.cmsa.go.tz)**

